**BUKU LA 21**

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb,

Ni vigumu kuamini kwamba tayari tumepita nusu ya mwezi wa kwanza wa 2021. Kitu ambacho si kigumu kuamini ni kiwango cha kujitolea na shauku ambayo kaunti yetu inayo katika kukabiliana na kila changamoto, kama vile Martin Luther King, Jr. Baada ya kusheherekea wiki ya kihistoria iliyojawa na Siku ya Martin Luther King, Jr na  Kuapishwa kwa Rais, ambapo kijana Malenga wa Ushairi wa kwanza wa kitaifa Laureate Amanda Gorman alikariri "**The Hill We Climb"** (**Mlima Tunaoupanda)**. Shairi hili la nguvu lilitukumbusha sisi sote kwamba licha ya jinsi mambo yalivyo au hata yanavyohisi, kuna mwamba wa matumaini na daima kuna maendeleo.

Ninakuhimiza ujiunge nami katika kuendelea kupata njia za kuishi, kupumua na kutekeleza matarajio na shauku kuwadia kuangazia mwanga kwenye mwamba huo wa matumaini katika hali zote.

Kama ujuavyo, mnamo Januari 11 tuliwasilisha taarifa kuhusu mpango wa kufungua tena shule wa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb (DCSD) wakati wa mkutano wa Bodi ya Elimu. Kwa kuzingatia uzito wa COVID-19 na kiwango cha juu cha maambukizi cha kaunti yetu, maamuzi ya makini yalifanywa kwamba wanafunzi HAWATARUDI kwa masomo ya ana kwa ana mnamo tarehe 19 Januari, kama ilivyoripotiwa awali.

Ninataka kuwahakikishia tena kila mtu kwamba taarifa ya wiki mbili itashirikiwa na familia kabla ya tarehe inayotarajiwa ya kurudi kwa wanafunzi katika masomo ya ana kwa ana kwa wanafunzi na wafanyakazi. Majengo yetu pamoja na timu zitaendelea kulenga kutekeleza mikakati ya kupunguza hatari na utayari wa shule ili kuhakikisha majengo yote yako tayari kupokea wanafunzi na wafanyakazi tukiweza kurudi darasani. Soma zaidi kuhusu mikakati hiyo hapa. Kumbuka: usalama wako wa jumla ndio kipaumbele chetu muhimu.

## Familia za DCSD

Asante kwa wazazi na walimu wetu wote waliotazama na kushiriki katika mkutano wetu wa hivi karibuni wa mtandaoni wa town hall. Tunashukuru kwa maoni yenu,

na umakini tunapotoa maelezo kuhusu mpango wa Wilaya wa kufungua shule tena. Ikiwa ulikosa mkutano huo wa town hall, tafadhali tembelea hapa kutazama:

Kiingereza: https://fb.watch/39hp97Mz96/
Kihispania: https://youtu.be/um9m5rDShPY

Kama nilivyosema katika mkutano wa town hall, wafanyakazi na waalimu wetu wakuu wa shule wanafanya kazi kwa bidii kuandaa jengo kwa masomo ya ana kwa ana. Tunatekeleza matembezi ya kila siku, tukifanya tathmini ya maeneo yanayohitajika kushughulikiwa na kukamilisha maagizo ya kazi.

Ijapokuwa bado haturudi kwa masomo ya ana kwa ana, tutaendelea kutekeleza mikakati tano muhimu ya kupunguza hatari ili kupunguza zaidi kiwango cha hatari ya maambukizi ya COVID-19 ndani ya shule. Mikakati hii ni:

- Matumizi sahihi na ya mara kwa mara ya barakoa
- Kutokaribiana na watu ikiwa inawezekana
- Kunawa mikono
- Kusafisha na kuua vidudu
- Kuwafuatilia watu waliokaribiana kwa kushirikiana na Bodi ya Afya ya DeKalb

Ni kwa mikakati hii kwamba tutaendelea kupanga kurejea darasani kwa usalama na kwa urahisi kwa wafanyakazi wetu na wanafunzi wetu. Ijapokuwa ninaelewa nyakati hizi zinabadilika mara kwa mara, nina imani kamili na kila mmoja yenu—timu, uongozi, bodi, na wanafunzi wetu wa ajabu—na asante kwa uwezo wako wa kuweza kubadilika na uwazi wa fikra.

Sisi sote tunaelewa kwamba nyakati hizi ni tofauti kabisa. Kwa familia zetu, tunaelewa mahitaji ya kupokea mawasiliano wazi, thabiti na mapya. Kitovu chetu cha Kufungua Shule Tena kinapaswa kuwa kituo chako cha kwanza kwa taarifa zote kuhusu mpango wa kufungua shule tena wa DCSD. Kwenye kitovu hivi, utajifunza kila kitu kuanzia matangazo, itifaki za usalama, taarifa za usafiri, masomo ya mtandaoni na hata lishe. Ninahimiza kila familia kualamisha na kuangalia tovuti ya kufungua shule tena mara kwa mara kwa taarifa.

**<u>Ratiba ya Masomo Kuanzia Januari 19, 2021</u>**

Asante kwa maoni yako kuhusu ratiba ya masomo. Ufafanuzi ulitolewa kwa waalimu wakuu na wafanyakazi katika maandalizi haya ya mpito. Urahisi wa kubadilika ni muhimu wakati huu.

Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb (DCSD) inarekebisha ratiba ya masomo ya mtandaoni kuanzia tarehe 19 Januari, 2021. Mpito hadi ratiba ya darasa la kawaida utaruhusu muda zaidi wa masomo kwa wanafunzi wote. Ratiba ya kila siku itatenga muda wa vyakula (kiamsha kinywa na chakula cha mchana) na mapumziko ya teknolojia. Madarasa yatafanyika Jumatatu, Jumanne, Alhamisi, na Ijumaa. Waalimu na wanafunzi wote watatumia Jumatano kama siku ya msaada wa masomo wa kuwaruhusu wanafunzi kupokea msaada, marekebisho, na/au uchapuzi wa masomo ya kibinafsi au katika mazingira ya kundi ndogo ya wanafunzi na walimu.

Bila kuhusisha Shule ya chekechea, ratiba iliyo hapa chini inawakilisha idadi ya chini ya dakika ambazo wanafunzi watapokea masomo ya moja kwa moja kutoka kwa waalimu wao. Viongozi na waalimu wa shule wanaweza kuongezea muda wa kusoma ana kwa ana kama inavyohitajika ili kuwasaidia wanafunzi. Wanafunzi wataendelea kushiriki katika kazi za kibinafsi na za kundi ambazo zinazidi muda uliowekwa wa masomo ya ana kwa ana.

| **KIWANGO CHA GREDI** | | **MUDA WA MASOMO YA ANA KWA ANA** |
|---|---|---|
| Shule ya Chekechea | | Saa 1 hadi saa 1 ½ kwa siku kwa kila DECAL |
| Shule ya msingi | Gredi K-2 | Dakika zisizopungua 15 kwa kila somo |
| Shule ya msingi | Gredi 3-5 | Dakika zisizopungua 20 kwa kila somo |
| Katikati | Gredi 6-8 | Dakika zisizopungua 30 kwa kila somo |
| Shule ya Upili | Gredi 9-12 | Dakika zisizopungua 30 kwa kila somo |

## Mtazamo wa Kalenda ya Wanafunzi ya Januari

Katika maandalizi ya kuanza muhula wa pili, tafadhali kagua mtazamo wa kalenda ya wanafunzi ya mtoto wako. Wanafunzi watahudhuria shule mtandaoni kuanzia tarehe 19 Januari, 2021. Tafadhali kumbuka kwamba Jumatano, Januari 20, imetengwa kama siku ya masomo ya mbali kwa wanafunzi.

**Januari 2021**

| Jumapili | Jumatatu | Jumanne | Jumatano | Alhamisi | Ijumaa | Jumamosi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **1** | **2** |
| **10** | **11**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi<br>Mitihani ya Mwisho | **12**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi<br>Mitihani ya Mwisho | **13**<br>Siku ya Masomo ya Kujitegemea kwa Wanafunzi<br>Mwisho wa Shughuli za Semesta | **14**<br>Siku ya Kazi ya Waalimu/Wafanyakazi<br>Shule Zinafungwa | **15**<br>Shule Zinafungwa | **16** |
| **17** | **18**<br>Sikukuu ya Dr. Martin L. King, Jr.<br>Shule Zinafungwa | **19 ~**<br>**Muhula wa Pili**<br>(Mwanzo wa ratiba kamili)<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **20 +**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **21**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **22**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **23** |
| **24** | **25**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **26**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **27**<br>Siku ya Masomo ya Kujitegemea kwa Wanafunzi | **28**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **29**<br>Siku ya Masomo ya Mbali kwa Wanafunzi | **30** |
| **31** | **~Kumbuka: Januari 19, 2021 – Wafanyakazi na wanafunzi watafuata ratiba ya masomo kama ilivyochapishwa katika Infinite Campus.**<br>**+ Kumbuka: Januari 20, 2021 – Wanafunzi watashiriki katika siku ya masomo ya mbali. Siku hii itatumika kama siku ya masomo ya kujitegemea.** | | | | | |

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu ratiba ya mtoto wako au kalenda ya mwanafunzi, tafadhali wasiliana na mwalimu mkuu, mwalimu, au mshauri wa mtoto wako.

## Taarifa ya Mtihani

Kama matokeo ya janga la sasa, lazima Wilaya ihakikishe kwamba mitihani imetekelezwa kwa njia ambayo itaendelea kuwaruhusu wanafunzi wetu kuwa salama na wenye afya huku tukitii maagizo ya Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC), Bodi ya Afya ya Kaunti ya DeKalb na Idara ya Elimu ya Georgia.

**Kulingana na Idara ya Elimu ya Georgia (GaDOE), mitihani yote inayofadhiliwa na jimbo, ikiwemo ACCESS na Mitihani ya Georgia Milestones, lazima itekelezwe ana kwa ana ili kukidhi maagizo ya serikali. Ikiwa wazazi watachagua mtoto wao kutoshiriki katika vikao vya mitihani vya ana kwa ana, tafadhali wasiliana na shule ya mtoto wako ili kujadili athari ya kutoshiriki.**

Hatua za Majira ya Baridi ya Utekelezaji wa Maendeleo ya Kielimu (MAP) zimepangwa kuwa Januari 4 - Februari 26, 2021. Katika mazingira ya kusoma kwa mbali, wanafunzi watapewa mtihani wa MAP mtandaoni kwenye kifaa kilichotolewa na wilaya au cha kibinafsi. Hata hivyo, kwa sababu ya hali ya mitihani ya MAP ya majira ya baridi, wanafunzi watapewa mtihani wa MAP katika mifumo miwili tofauti ya mitihani: kwa mbali (Sayansi na Matumizi ya Lugha) **na** ana kwa ana (Hisabati na Kusoma). **Ikiwa wazazi watachagua mtoto wao asishiriki katika vikao vya mtihani vya ana kwa ana, mtoto hatafanya sehemu hizo kwa wakati huu.**

**HONGERA!!**
**Kwa Mwenyekiti Wetu Mpya wa DCSD + Mwenyekiti Msaidizi**

Hongera kwa Mwenyekiti wa Bodi aliyechaguliwa bila kupingwa, Bi. Vickie B. Turner na Bw. Diijon DaCosta, aliyechaguliwa bila kupigwa kuwa Mwenyekiti Msaidizi na Bodi ya Elimu ya Kaunti ya DeKalb.

Bi. Tuner, mwanachama mtendaji katika Kaunti ya Dekalb kwa miaka 20, amejitolea kwa elimu ya umma kwa miaka 24. Pamoja na kuhudumu katika Wilaya ya 5 kwa zaidi ya miaka 6, Bi. Turner ana shauku kuhusu kutumia tajriba na shauku yake katika jamii na elimu katika kazi yake mpya.

Bw. Diijon DaCosta alijiunga na DCSD mwaka wa 2014 kama mwalimu kabla ya kuanza kuhudumu katika Wilaya ya 6 mnamo mwaka wa 2018. Kama kiongozi mwenye shauku kuhusu ufanisi wa elimu kati ya vijana, ana furaha kuhusu kutoa mtazamo mpya na msaada wazi katika jukumu lake mpya.

Nina furaha sana kuhusu viongozi hawa wa ajabu na jinsi watakavyoongoza bodi na jamii yetu kuwadia hatua nzuri na zenye maendeleo.

Ningependa pia kumshukuru Mwenyekiti wa Bodi anayeondoka Bw. Marshall Orson kwa huduma na uongozi wake.

Pia, huku nikituma pongezi, ningependa kuwapa pongezi Wanachama wa Bodi ya Elimu ya DCSD kwa kuchaguliwa tena katika nyadhifa zao. Ninataka kuwashukuru mimi binafsi kwa kujitolea kwenu kwa wilaya yetu, shauku yako kwa wanafunzi na wafanyakazi wetu na msaada wenu unaoendelea kwangu na timu mbalimbali ambazo unafanya kazi nazo kila siku. Ili kumwona kila Mwanabodi tembelea hapa.

**Maombi ya Hali Ngumu**

Kama mfanyakazi wa DCSD, tunataka kumshukuru kila mfanyakazi ambaye amerudi katika majengo yetu. Tunaelewa kwamba afya na maslahi yako ni muhimu sio tu kwa wilaya na wanafunzi wetu lakini pia kwa familia yako mwenyewe. Baada ya kusikia kutoka kwako, tunataka kuwatambua wale kati yenu walioonyesha hitaji la kazi mbadala kwa sababu ya ugumu. Maombi yetu ya hali ngumu - ambayo yalipaswa kuwasilishwa kabla ya Januari 8 - yalikuwezesha kuandika wasiwasi unao na kurudi kwenye jengo au ratiba ya kazi yako, na yatatekelezwa hadi Februari 2, 2021.

Haijalishi sababu yako ya ombi la hali ngumu, ni tumaini letu kwamba wakati wa kipindi cha siku 20 utafanya mipangilio inayofaa ya kibinafsi kurudi tarehe 2, Februari 2021.

Kwa hakika, ikiwa una wasiwasi au hali ya kuripoti kabla ya tarehe 3 Februari, tafadhali wasiliana na msimamizi wako.

Tena, asante sana kwa kazi yako ngumu inayoendelea katika kila kitu unachokifanya wakati wa nyakati hizi zisizo na kifani.

Kwa kutamatisha, ninataka kuwashukuru nyote kwa bidii, uvumilivu, na subira. Ninataka pia kutoa shukrani maalum kwa Kamati yetu Kuu ya Ushauri wa Wanafunzi (SSAC) na msemaji mgeni German DuBois III ambaye nilikutana naye wiki hii. Ninashukuru kwa vipengele vilivyoibuliwa kuhusu mwongozo wa vilabu vya

wanafunzi na muda wa skrini na ratiba mpya. Ninatazamia mikutano zaidi na wanafunzi wetu werevu.

Ninapofikiria kuhusu kazi ngumu unayowafanyia wanafunzi wetu, nukuu hii ya Martin Luther King, Jr. Inanijia akilini. “Swali la kudumu na la haraka zaidi maishani ni: “Unawafanyia wengine nini?” Unaishi na kupumua ufafanuzi wa inamaanisha nini kutokuwa mbinafsi na mwenye shauku. Asante kwa kuendelea kuja kila wakati, mwaka baada ya mwaka. Wanafunzi, wasimamizi, wafanyakazi, na wilaya yetu inakushukuru.

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris